# BODI YA KOROSHO TANZANIA

## TANGAZO KWA WADAU WOTE WA TASNIA YA KOROSHO NCHINI

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) inapenda kuwataarifu wadau wote wa Tasnia ya Korosho nchini kwamba Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Mohamed Bashe ametoa kibali cha korosho ghafi kusafirishwa kwa muda wa saa 24 kuanzia leo tarehe 24/10/2024 hadi tarehe 15/11/2024. Ruhusa hii imetolewa maalum kwa ajili ya: -

i. Kupunguza mlundikano wa korosho ghafi katika ghala kuu ili kuruhusu korosho kutoka vyama vya msingi kuingia ghalani kwa wakati;
ii. Kuongeza mzunguko wa malori yaliyopo katika kusafirisha korosho ili kupunguza changamoto ya uhaba wa magari;
iii. Kuwawezesha wanunuzi kuwahi meli katika Bandari ya Mtwara.

Aidha, ruhusa hii imetolewa kwa korosho zinazosafirishwa kutoka ghala kuu zilizopo mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma kwenda Bandari ya Mtwara au katika ghala za kuhifadhi korosho zilizopo Mtwara. Hata hivyo ili kuongeza udhibiti wa ubora wa korosho usafirishaji wa korosho ghafi kutoka kwenye Vyama vya Msingi (AMCOS) kwenda Ghala Kuu pamoja na upokeaji/upakiaji wa korosho katika ghala kuu utaendelea kufanyika kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni, kama ilivyo katika Mwongozo Na.1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi kupitia Stakabadhi Ghalani Msimu 2024/2025.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**